# Jifunze Zaidi kuhusu Programu za Qualcomm

Makampuni tanzu ya Qualcomm yanatoa programu na huduma mbalimbali ili kusaidia kuboresha utendakazi wa kifaa cha mkononi, kusaidia kuhifadhi nguvu ya betri, na kusaidia kuboresha usalama wa kifaa.  Pogramu hizi ni kama zifuatazo:

**Qualcomm Location**

Qualcomm Location (iliyokuwa “IZat”) ni teknolojia inayotolewa na Qualcomm Technologies, Inc. nchini Marekani., QT Technologies Ireland Limited katika nchi za Maeneo ya Kiuchumi ya Ulaya, na  Qualcomm CDMA Technologies (Korea) YH katika Jamhuri ya Korea (inayojulikana kama Korea Kusini).  Qualcomm Location inaweza kuwezesha kifaa chako kubainisa eneo lake kwa haraka na kwa usahihi zaidi – hata wakati kifaa chako hakiwezi kupata ishara thabiti ya GPS. Qualcomm Location inaweza pia kusaidia kifaa chako kuhifadhi nguvu ya betri wakati unatumia programu au huduma zinazohitaji data ya eneo.  Ikiwa unatumia programu zilizowezeshwa eneo, huenda kifaa chako kikahitaji kutuma eneo lake kwa watoa huduma hao wa programu.  Maelezo ya eneo yaliyotolewa kwa watoa programu husimamiwa na masharti yao na sera za faragha. Tunapendekeza urejelee masharti na sera za faragha za watoa huduma hao wa programu.

Mara kwa mara Qualcomm Location hupakia data kwenye kifaa chako kuhusu maeneo ya minara iliyo karibu ya simu na maeneo ya ufikiaji ya WiFi. Huenda data hii ikachanganywa na data kutoka kwa sensa kwenye kifaa chako kama bile groskopu au aseleromita ili kusaidia kifaa chako kubainisha eneo lake na kuhifadhi nguvu ya betri.

Mara kwa mara Qualcomm Location hututumia kitambulisho cha kipekee cha programu, eneo la kifaa chako (longitudo, latitudo na mwinuko, na kutokuwa na uhakika) na minara iliyo karibu ya simu na maeneo ya Wi-Fi, nguvu ya ishara, na saa (kwa pamoja, "Data ya Eneo"). Kama vile muunganusho wowote wa Intaneti, tunapokea pia anwani ya IP ambayo kifaa chako hutumia. Tunatumia pia Data ya Eneo, Vitambulisho vya programu na anwani za IP, na data nyingine tunayokusanya ili kukusaidia kulinda, kutathmini, na kuboresha utendakazi wa mifumo yetu.

Qualcomm Location hutumia hatua mbalimbali mwafaka na zinazofaa za usalama kulinda data tunayokusanya. Kwa kuongezea, hatuhifadhi kabisa Data ya Eneo na kitambulisho cha programu yako au anwani ya IP, au hatujaribu kuwatambua watumiaji wa Qualcomm Location. ili kuboresha utendakazi wa mfumo wa kitambulisho cha programu yako na anwani ya IP inayohusishwa na Data ya Eneo lako kwa siku thelathini kuanzia kupokea ambapo itafutwa kabisa. Baada ya kuondoa anwani za IP na vitambulisho vya programu, tunakusanya Data ya Eneo ili kuunda hifadhidata bila jina inayohusiana na maeneo ya minara ya simu na maeneo ya ufikiaji ya WiFi.

Ikiwa uko katika Jamhuri ya Korea, huduma ya Qualcomm Location huafikiana na Sheria ya Ulinzi wa Maelezo ya Maeneo ("Sheria") na una haki ya haki husika chini ya Sheria hii.  Kwa maswali au maoni kuhusu kanuni zetu nchini Korea, tafadhali wasiliana nasi kwenye:

Qualcomm CDMA Technologies (Korea) YH
Attention Legal Department
4th, 15th, 16th & 17th Fl.
119, Nonhyeon-dong, Gangnam-gu
Seoul, 135-820
Republic of Korea
Nambari ya Simu: 82-2-3404-1114

**Ripoti za Qualcomm Technology (QTR) -- Takwimu za Uchunguzi**

QTR ni teknolojia inayotolewa na Qualcomm Technologies, Inc. nchini Marekani, na QT Technologies Ireland Limited katika Maeneo ya Kiuchumi ya Ulaya.  QTR inaweza kukusanya: (i) majina ya programu zilizosakinishwa na/au kuendeshwa kwenye kifaa (ii) maelezo ya usanidi (kama vile muundo, modeli, mfumo wa uendeshaji na toleo, programu msingi na matokeo, mtoa huduma ya pasiwaya, msimbo wa nchi ya simu ya mkononi na msimbo wa mtandao, na nambari tambulishi ya chipseti (ambayo haikutambui)), (iii) takwimu za utendakazi na usalama wa kifaa (kama vile CPU, GPU, au utendakazi wa modemu), na (iv) data ya sensa ambayo haitakutambua, lakini inayopima mwenendo, mwelekeo, na hali za mazingira kwenye simu. Data imepakiwa kupitia WiFi iliyofichamishwa, au katika viwango vidogo, kupitia mtandao wako wa simu.

Tunatumia QTR ya data kukusanya kwa malengo yaliyofafanuliwa katika Sera hii, ikiwa ni pamoja na kutusaidia kukuza teknolojia mpya za vifaa vya mkononi ili kuboresha utendakazi wa pasiwaya, kuhifadhi nguvu ya betri, kukuza hatua za usalama, na kuboresha shughuli za biashara yetu.  Tunaweza pia kushiriki data ya QTR na watoa huduma wa pasiwaya au watengeneza vifaa ili kuwasaidia kuboresha vifaa, mitandao, na usalama wa pasiwaya.

QTR hutoa chaguo la kutoshiriki katika ukusanyaji wa data katika menyu ya mipangilio ya Android chini ya kichwa cha, "Ripoti za Qualcomm Technologies".  Kuchagua kutoka hakutaathiri vibaya utendakazi wa kifaa chako.

<u>Vidokezo vichache</u>:    Kama vile muunganisho wowote wa intaneti, tutapokea anwani ya IP ambayo kifaa hutumia, lakini tutaifuta mara moja baada ya kuipokea.  Kama QTR itatutumia data yoyote isiyotambuliwa katika sera hii ya faragha ambayo inaweza kuwa data ya kibinafsi, sisi huifata data hiyo mara moja baada ya kuipokea.  Baadhi ya matoleo ya QTR huwa pia na uwezo wa kukusanya "kitambulisho cha  kimataifa cha vifaa vya Mkononi (IMEI) cha kifaa, lakini uwezo huu hautumiki kwa sasa.  Ikiwa baadaye, tutakusanya IMEI, itakusanywa kwa malengo yaliyofichuliwa na muhimu, na kulingana na sheria zote husika za ulinzi na faragha ya data. Mwishowe, baadhi ya matoleo ya QTR yana pia uwezo wa kukuruhusu kuchagua kushiriki katika kututumia data ya eneo la kifaa.  Ukichagua kushiriki katika kututumia data ya eneo, tunaweza kukusanya mara kwa mara eneo la kifaa chako ili kutusaidia, kwa mfano, kutambua maeneo yenye mtandao wa pasiwaya yasio na ishara ya kutosha.

**Snapdragon Smart Protect**

Qualcomm® Snapdragon™ Smart Protect ni huduma ya programu ya vifaa ya Android (“Smart Protect”) imeletwa kwako na QT Technologies Ireland Limited katika Maeneo ya Kiuchumi ya Ulaya na Qualcomm Technologies, Inc. nchini Marekani. Smart Protect hufuatilia tabia ya programu za Android kwenye kifaa ambacho kimesakinishwa, na hutumia tabia za mashine kutambua tabia za kuarifu za programu hasidi, programu chakura, programu za matangazo, na programu mbaya. Smart Protect huripoti tabia kama hizo kwa programu za usalama za wateja wetu zilizosakinishwa kwenye kifaa kimoja.

Ili kusaidia kuboresha Smart Protect, na matumizi mengine tuliyoyafafanua katika Sera hii ya Faragha, Smart Protect hututumia muhtasari wa ugunduzi wa programu hasidi pamoja na jina la programu na shughuli zake zinazosababisha arifa, data msingi kuhusu kifaa kama vile muundo, modeli, na toleo la mfumo wa uendeshaji, na data kuhusu usanidi wa kifaa kama vile mpangilio wa lugha, mtoa huduma, na msimbo wa nchi.

**Vellamo**

Vellamo ni programu ya utathmini ya vifaa vya Android (“Vellamo”) inayoletwa kwako na Qualcomm Innovation Center, Inc. Vellamo huchanganua na kuripoti utendakazi wa mfumo wa kifaa ambacho kimesakinishwa. Unaweza pia kuchagua kulinganisha utendakazi wa kifaa chako na vifaa vingine tulivyovijaribu na, kwa kufanya hivyo, huenda kifaa chako kikatutumia matokeo ya majaribio na maelezo ya mfumo.  Huenda maelezo kama hayo ya mfumo yakajumuisha: jina la mtengenezaji wa kifaa, modeli na toleo; maelezo kuhusu maunzi kwenye kifaa chako kama ile kichakataji, kumbukumbu, na sensa zinazopatikana, aina na toleo la mfumo wa uendeshaji; maelezo ya uonyesho; anwani ya itifaki ya intaneti, wakala wa mtumiaji wa kivinjari, na maelezo kuhusu mtandao wa simu ambao kifaa huunganisha. Tunatumia data tunayokusanya kwa lengo lililofafanuliwa katika Sera hii, ikiwa ni pamoja na huduma za utathmini wa utendakazi unaoomba na kuchanganya takwimu 'halisi' kuhusu utendakazi wa kifaa cha mkononi.

**Data Iliyobashiriwa ya Mzunguko wa Setileti ya GNSS ya – XTRA**

XTRA ni teknolojia inayotolewa na Qualcomm Technologies, Inc. nchini Marekani na QT Technologies Ireland Limited katika Maeneo ya Kiuchumi ya Ulaya ili kuboresha utendakazi wa kifaa cha mkononi.  XTRA hupakua faili ya data kutoka kwa Qualcomm yenye mizunguko iliyobashiriwa ya Setileti za Mfumo wa Setileti za Urambazaji za Ulimwengu (GNSS). Kutumia faili ya data ya XTRA hupunguza muda ambao kifaa uhitaji kuhesabu eneo lake, kwa hivyo kuokoa muda na nguvu ya betri wakati wa kutumia programu za maeneo. Matoleo mapya ya programu ya XTRA hupakia pia kiasi kidogo cha data kwetu. Tunatumia data iliyopakiwa kwa malengo yaliyofafanuliwa katika Sera hii, kama vile kudumisha na kuboresha ubora, usalama, na uadilifu wa huduma. XTRA hupakia aina zifuatazo za data: kitambulisho cha kipekee kinachozalishwa bila mpangilio maalum, jina la chipseti na nambari tambulishi, toleo la programu ya XTRA, msimbo wa nchi ya simu na msimbo wa mtandao (inayoruhusu utambuaji wa nchi na mtoa huduma wa simu), aina ya mfumo wa uendeshaji na toleo, muundo wa kifaa

na modeli, muda tangu kuwashwa kwa kichakataji cha programu na modemu, na orodha ya programu zetu kwenye kifaa.